Muhammad
(s.a.w)
Ni Nani?
www.islamic-invitation.com

Muhammad (s.a.w) Ni Nani?

Waislamu wanaamini kwamba Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) ndiye mwisho wa Mitume waliotumwa ili kuwalingania viumbe wamtii Mwenyezi Mungu peke yake na kumuabudu, na miongoni mwa Mitume hao ni Adam, Nuh, Ibrahim, Ismail, Is-haq, Yaqub, Yusuf, Mussa, Daud, Suleyman na Issa (amani ya Allah iwe juu yao).

Kama alivyotumwa Nabii Mussa (a.s) na Taurat iliyo sahihi ambayo haijabadilishwa, vilele Nabii Issa na Ijili iliyo sahihi ambayo haijabadilishwa, basi alitumwa Muhammad (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) na Qur'an ili iwaongoze watu na iwahukumu.

Aliulizwa Mama Aisha (r.a) mke wa Mtume (s.a.w) kuhusu sifa za Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake), akasema: "alikuwa Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) ni Qur'an inayotembea ardhini".

{Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana}. (Al-Ahzab: 21).

Na tunaelezea miongoni mwa sifa zake Mtume (s.a.w) za vitendo.

Ujumbe wa rehma

Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) Kama alivyowafundisha watu kuswali, kufunga na kutoa Zakka, vilevile aliwafundisha tauhidi na kuishi na watu vizuri, amesema Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake): "Mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho basi asimuudhi jirani yake, na mwenye kumuamini Mwenyezi

Mungu na siku ya mwisho na amkirimu mgeni wake, na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na aseme yaliyo ya kheri au anyamanze".

Na vilevile aliwafundisha watu huruma na kuwaheshimu wengine, amesema Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake): "Mtu asiye na huruma naye hahurumiwi". Na katika hadithi nyingine, watu walimuomba Mtume (s.a.w) awaombee dua mbaya washirikina akasema: "Hakika mimi sikutumwa niwalaani watu, bali nimetumwa niwe rehma kwa watu".

{Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote}. (Al-Ambiyaa: 106).

Kusamehe

Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) alikuwa ni mwingi wa kusamehe na alikuwa rafiki wa watu, anapoudhiwa alikuwa akisubiri na anamsamehe yule aliye aliye muudhi.

Na unadhihiri upole wa Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) ni kwamba alikuwa ana uwezo wa kuhukumu na kulipiza maudhi, pamoja na hayo Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) alipata maudhi na hakuya nyamanzia, lakini alikuwa anayasamehe, akawa ni mfano wa kuigwa katika kusamehe na upole kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Shikamana na kusamehe, na amrisha mema, na jitenge na majaahili}. (Al-A'araaf: 199).

{Na wasamehe, na waachilie mbali. Je! Nyinyi hampendi Mwenyezi Mungu akusameheni? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu}. (Al-Nnuur: 22).

Usawa

Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) alikiri kwa Aya hii ya kwamba viumbe wote wako sawa mbele ya Mwenyezi Mungu, amesema Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake): "Nyinyi wote mmetokana na Adam, na Adam ametokana na mchanga, hakuna ubora kwa mwarabu juu ya muajemi, wala mtu mwekundu juu ya mtu mweusi, isipokuwa kwa ucha Mungu".

Na amesema pia: "Hakika Mwenyezi Mungu haangalii kunako miili y enu wala sura zenu, lakini anatizama nyoyo zenu na matendo yenu".

Na imepokelewa kwamba mmoja katika Maswahaba alimtukana mwenzake akamwambia ewe mtoto mweusi, Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) akamwambia: "Ewe Aba Dharri umemtukana kwa sababu ya mama yake? Hakika wewe ni mtu mwenye mambo ya kijahili".

{Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi}. (Al-Hujraat: 13).

Msamaha

Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) aliwafundisha waislamu wasilipize maudhi kwa wale walio waudhi, bali wasamehe na wapuuze, na wawatendee wema wale waliowafanyia ubaya.

Na vitabu vya kiislamu vimekusanya mifano mingi katika hilo, Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) na uwezo wa kuchukua haki yake kwa yule aliye mdhulumu, lakini alisamehe na kupuuzia, na aliwafundisha Maswahaba juu ya kufanya subra wakati wa shida, amesema Mtume (rehma na amani za Allah

ziwe juu yake): "Mtu shajaa sio kwa kupigana, bali shujaa ni yule anaeimiliki nafsi yake wakati wa hasira".

Subra na kupuuzia haimaanishi ni kumtelekeza muislamu na matatizo yake wakati wa maudhi, isipokuwa ni kama alivyosema Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake): "Msitamani kukutana na maadui, na mkikutana nao fanyeni subra".

{Mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa lilio jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu}. (Fusswilat: 34).

Ulaini

Amesema Anas bin Malik (r.a): "Nilimtumikia Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) miaka kumi, hajawahi kuniambia 'uff' wala hakuniambia kwanini umefanya wala kwanini hujafanya".

Na kutoka kwa Aisha (r.a) mke wa Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) alisema: "Liliingia kundi la Mayahudi kwa Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) wakasema: Assaam alaykum, (kuangamia kuwe juu yenu) Aisha akasema: Nikaielewa kisha nikasema: alaykum ssaamu wa laana (kuangamia kuwe juu yenu na laana), Aisha anasema: Akasema Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake): Taratibu ewe Aisha, hakika Mwenyezi Mungu anapenda upole katika mambo yote, nikasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu hukusikia walivyosema? Mtume akajibu: Nimesema wa alaykum (na kuwe juu yenu kuangamia), na akasema Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake): Ewe Aisha kuwa mpole, hakika ya upole hauwi katika jambo isipokuwa unalipamba, na hauondolewi upole katika jambo isipokuwa linaharibika".

{ Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao. Na lau ungeli kuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangeli kukimbia}. (Al-Imran: 159).

Kunyenyekea

Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) alikuwa hapendi kusimamiwa kwa ajili ya kunyenyekewa, na katika kikao alikuwa anakaa sehemu walipoishia watu (hakuwa akiachiwa nafasi) na akikaa sehem ya kawaida na wala si mahala pa kuinuka (akawa juu ya engine), na alikuwa havai nguo zinazomtofautisha na Maswahaba zake, au aonekane katika daraja la juu kuliko Maswahaba.

Na Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) alikuwa anachanganyika na mafakiri na masikini, na akikaa na wazee na akiwasaidia wajane.

Na alisema Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) kuwambia Maswahaba zake: "Hakika Mwenyezi Mungu ameniteremshia wahyi ya kwamba muwe wanyenyekevu ili asijifakharishe mmoja wenu juu ya mwingine, na ili mtu asimfanyie uovu mwenzake".

Na alikuwa Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) akinyenyekea kwa kuchelea asiabudiwe pamoja na Mwenyezi Mungu, au kufanywa Mungu, akasema: "Msinitukuze kama wakristo walivyo mtukuza Issa bin Mariyam, hakika mimi ni mja, basi semeni mja wa Mwenyezi Mngu na Mtume wake".

{Na waja wa Arrahman Mwingi wa Rehema ni wale wanao tembea ulimwenguni kwa staha, na wajinga wakiwasemeza hujibu: Salama!}. (Al-Furqaan: 63).

Mume bora

Alisema Aisha mke wa Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) na ni mke anaependwa sana na Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake): "Mtume (s.a.w) Alikuwa anaitumikia familia yake, na akishona nguo, akisafisha viatu vyake, akikamua maziwa, akikanda unga na akiwalisha wanyama wake".

Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) hakuwa ni mume mwenye ikhlas tu, bali alikuwa akiwahimiza Maswahaba zake wamuige yeye, akasema: "Waumini wenye imani iliyo kamilika ni wale wenye tabia njema, na mmbora wenu ni yule mmbora kwa mke wake".

{Na kaeni nao kwa wema}. (Annisaa: 19).

Kiigizo chema

Yaliyotangulia ni mtizamo kuhusu maisha ya Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake), na yale yaliyotajwa miongoni mwa mifano ikiwemo huruma na upole yanaweza yakawashangaza baadhi ya watu kwa kuathirika kwao kutokana na mtizamo wa vyombo vya habari na maudhi yanayoupata uislamu kutokana na kuchafuliwa.

Ukitaka kuufahamu uislamu kwa ufahamu sahihi, basi uchukue uislamu kutoka katika vitabu vyake, na usiuhukumu uislamu kutokana na vitendo vya baadhi waislmu.

{ Na hakika wewe una tabia tukufu}. (Al-Qalam: 4).

Rai za wasiokuwa waislamu kuhusu Mtume (s.a.w)

Mahatima Gandhi: Ni kiongozi wa kisiasa na wa kirohani wa harakati ya Editorial (tahriri) ya Kihindi: "Nimetaka nijue sifa za

mtu ambae anamiliki bila upinzani nyoyo za mamilioni ya watu, nimetosheka ukweli wa kutosheka ya kwamba upanga haukuwa ndio njia ambayo kwa kupitia njia hiyo uislamu ulipata cheo, bali cheo cha uislamu kilipatika kupitia unyenyekevu wa Mtume (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) na usahihi wake na ukweli wake katika ahadi, na ubunifu wake na kuwa na ikhlas kwa rafiki zake na wafuasi wake, na ushujaa wake pamoja na kujiamini katika kumtegemea Mola wake na katika ujumbe wake, sifa hizi ndizo zilizo mtengenezea njia na kumvusha katika matatizo na wala sio upanga".

George Bernard Shaw: "Hakika ulimwengu kiukweli unamuhitaji mtu mwenye akili kama za Mtume Muhammad (rehma na amani za Allah ziwe juu yake), na watu wa dini katika karne za katikati walichora picha yenye giza ikimuhusu Mtume Muhammad (rehma na amani za Allah ziwe juu yake) kwa sababu ya ujinga na ubaguzi wao, na walimchukulia kuwa ni hatari kubwa kwa ukristo.

Baada ya kusoma historia yake nimekuta ni mtu mwenye kushangaza, na nikagundua kwamba hakuwa ni adui wa ukristo kamwe, bali inapasa apewe sifa ya kwamba ni mkombozi wa wanadamu, na ninavyoona kwa rai yangu, akipewa utawala anaweza akatatua matatizo yote ya ulimwengu, na ataleta mafanikio na amani ambayo inatamaniwa na wanadamu.

Muhammad (s.a.w) Inapasa Umjue Mtu Huyu